

Uhuru ng'o kwa Makoloni —Salazar

Lisbon, Ureno, Jumanne.

WAZIRI MKUU wa Ureno, Antonio de Oliveria Salazar, amesema leo kuwa hatakubali hata kidogo kutoa uhuru wa nchi ya Msumbiji, Angola na Portuguese Guinea; na yuko tayari kwa hali yote yote kulinda makoloni yake hayo.

Salazar amesema hayo kati-ka mashambulio yake makafi aliyotoa kwa Umoja wa Mata-ifa na nchi huru za Kiafrika.

Waziri Mkuu huyo Salazar mwenye umri wa miaka 74, na aliyetawala Ureno kwa miaka 30, ametoa matamshi yake hayo katika redio na televisheni kwa mara ya kwa-nza tangu koloni lake la Goa kutekwa na India.

Kiafrika

Salazar katika hotuba yake amedai kuwa Ureno pia ni nchi ya Kiafrika inayojitahidi kujenga taifa la mseto na wala haina kusudio la kukubali madai ya "utalifa mweusi".

Aliongeza kusema kuwa nchi hizo za Angola, Msumbiji na Guinea, siyo Makoloni ya Ureno, ila ni Majimbo yake, hivyo nchi hizo ni sehemu ya Ureno.

Akaendelea kusema kuwa Ureno itatumia kila sehemu ili kulinda 'majimbo yake hayo'

Mwafrika
14/8/63